

Mh. Mwenyekiti hadi tarehe 30/08/2017 Halmashauri ilitakiwa kuwa imekusanya 16.6% katika vyanzo vyake vya ndani. Kwa sasa tumekusanya 14.2 na tuko nyuma kwa 2.4%. Jedwali lifuatalo linaonyesha baadhi ya vyanzo ambavyo havikufikia lengo.

Na.	Chanzo cha mapato	% Iliyofikiwa		Sababu za kutofikia lengo	Mikakati ya kufikia lengo
1	Ushuru wa Magulio	9.08	AFISA MAPATO	Idadi ya wafanyabiashara kupungua kwenye baadhi ya magulio kutokana na hali ya uchumi kusuasua	Kuendelea kutoa elimu kwa wafanyabiashara kwamba kwa kile wanachouza wanapaswa kulipa ushuru kwa Halmashauri ili kiweze kutumika kutoa huduma kwa jamii.
2	Ada ya Matangazo	1.35	MHANDISI UJENZI	Utafiti ulikuwa haujafanyika kujua idadi na ukubwa wa mabango yaliyopo katika wilaya	Hati za madai zimesambazwa kwa wadaiwa na ufuatiliaji unaendelea aidha halmashauri imefungua kesi kwa kampuni za Pepsi,Cocacola, Tbl na kampuni zingine zenye mabango na kesi iko kwenye hatua ya kusikilizwa
3	Ushuru wa Mialo	4.61	AFISA UVUVI	Upatikanaji mdogo wa samaki katika kipindi hiki cha kiangazi	Kuongeza nguvu katika ukusanyaji na ukusanyaji unaendelea
4	Ushuru wa Vibanda/Nyumba	9.48	AFISA ARDHI	Baadhi ya Maeneo yaliyokusudiwa kutoza kodi hii ambayo ni: Usagara na ng'ombe bado taratibu zinaendelea.	Ufuatiliaji unaendelea kufanyika kupitia kwa watendaji wa kata , hata hivyo wadaiwa sugu hatua za kuwafungia zinachukuliwa

5	Ushuru wa Vinywaji Vikali	6.30	AFISA BIASHARA	Kwa mujibu wa sheria ya vileo msimu wa uhuishaji leseni hizo haujafika hadi Oktoba	Utaanza kukusanywa Mwezi Septemba 2017
6	Upimaji wa Viwanja	1.06	AFISA ARDHI	Wananchi hawajapimisha maeneo yao kwa kiwango kikubwa.	Uhamasishaji unaendelea kufanyika ili wananchi waweze kuchangia gharama za upimaji wa maeneo wanayomiliki
7	Leseni za Uvuvi	-	AFISA UVUVI	Leseni za uvuvi zinaanza kutolewa Mwezi Januari hadi Machi kila mwaka	Kufuatilia kwa karibu wadau ambao hawajalipa walipe kwa wakati .
8	Leseni za Vyombo vya Uvuvi	1.06	AFISA UVUVI	Leseni za uvuvi zinaanza kutolewa Mwezi Januari hadi Machi kila mwaka	Kufuatilia kwa karibu wadau ambao hawajalipa walipe kwa wakati hata hivyo wanaendelea kulipa.
9	Vibali vya Ujenzi	0.57	MHANDISI UJENZI	Mapato haya hutegemea kasi ya ujenzi ilivyo katika maeneo yaliyopimwa.	Kufanya kaguzi maeneo yote ambayo ujenzi unaendelea .
10	Shughuli za Madini	1.91	AFISA MAPATO	Baadhi ya makarasha na maduara kutozalisha au kufungwa	Kuweka nguvu ya ukusanyaji mara makarasha na maduara yanapozalisha ili kuondoa ukwepaji wa ulipaji wa ushuru.
11	Ushuru wa Nyumba za Kulala Wageni	6.80	AFISA BIASHARA	Ushuru umeanza kukusanywa kwa kuchelewa kutokana na tamko la Serikali	Tayari tumeanza kuzungukia nyumba za kulala wageni na kutoa elimu na tayari wameanza kulipa

12	Ushuru wa Minara ya Simu	-	AFISA MAPATO/SHERIA	Wamiliki wa Minara wanasuasua kulipia	Halmashauri imeboresha rejista ya Minara kwa sasa minara yote iliyopo kwenye Taasisi ikiwemo maeneo ya shule ,Zahanati na vijiji minara hiyo imejumuishwa katika daftali la Halmashauri na hati za madai ya minara yote 37 iliyopo Wilayani zimeshapelekwa kwa wamiliki na ufuatiliaji unaendelea.
13	Ada za Michezo na Utamaduni	-	AFISA UTAMADUNI	Watendaji wa kata/kijiji kutopewa elimu juu ya ada za michezo/utamaduni. Shughuli za kusanyiko kama harusi ni za msimu.	Watendaji tayari wameshapewa maelekezo ya namna na viwango vya utozaji wa ushuru. Ufuatiliaji kuhusiana na ada hizo zinaendelea